TANZANIA PRIVATE SECTOR FEDERATION



Chaguzi za Kisera

Mtazamo wa TPSF Kuhusu Kulinda Viwanda vya Ndani na Kuimarisha Sekta ya Uzalishaji wa Chuma Nchini Tanzania

"Kukuza Ushindani wa Haki, Ushiriki wa Wazawa na Ukuaji Endelevu wa Viwanda"


November, 2026


1. Utangulizi

Chuma ni moja ya malighafi muhimu katika maendeleo ya uchumi wa Tanzania kwa kuwa Kinatumika katika sekta mbalimbali zikiwemo ujenzi, usafirishaji, nishati, miundombinu ya maji, kilimo na viwanda. Hivyo, upatikanaji wa chuma na bidhaa za chuma zenye ubora kwa bei shindani ni muhimu katika kupunguza gharama za miradi, kuongeza ushindani wa viwanda na kuvutia uwekezaji. Kwa sababu hiyo, Mpango Elekezi wa Muda Mrefu wa Maendeleo wa Tanzania 2050 unatambua nafasi ya sekta ya viwanda katika kukuza uchumi, kuongeza uzalishaji, kupanua mauzo ya bidhaa nje ya nchi na kuvutia uwekezaji. Mwaka 2024, sekta ya viwanda ilikua kwa asilimia 4.8, ikichangia asilimia 7.3 ya Pato la Taifa na mauzo ya bidhaa za viwandani nje ya nchi yalifikia Dola za Marekani bilioni 1.34.

Katika kuunga mkono ajenda ya Serikali ya kujenga uchumi wa viwanda, sekta binafsi imeendelea kuwekeza kwenye sekta ndogo ya chuma. Kufikia Machi 2024, Tanzania ilikuwa na viwanda 28 vinavyozalisha chuma na bidhaa za chuma, vikiwemo viwanda 19 vya nondo vyenye uwezo wa kuzalisha takriban tani milioni 1.30 kwa mwaka. Aidha, takwimu zilizotolewa zimeonesha ongezeko la uwezo wa uzalishaji hadi tani milioni 2.70 mwaka 2025, huku upanuzi wa viwanda vikubwa vinne ukitarajiwa kuongeza uwezo huo hadi takriban tani milioni 4.38. Hali hii inaonesha uwekezaji unaoendelea katika sekta hii na fursa ya kuongeza uzalishaji wa ndani ili kukidhi mahitaji ya soko.

Kwa upande wa uzalishaji wa mabati, Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara ya mwaka 2026/27, iliyowasilishwa Bungeni tarehe 22 Mei 2026, ilieleza kuwa wazalishaji wakubwa watano wakiwemo Lodhia, MMI Steel, ALAF, Kinglion na GSM wana uwezo wa pamoja wa kuzalisha tani milioni 1.11 kwa mwaka, wakati mahitaji ya ndani yanakadiriwa kuwa tani 630,000. Uzalishaji ulifikia takriban asilimia 70 ya uwezo uliosimikwa, huku ziada ya mabati ikiuzwa katika masoko ya nchi jirani, zikiwemo Burundi, Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Malawi. Haya ni mafanikio yanayoonesha kuwa wazalishaji wa ndani wana uwezo wa kuhudumia soko la Tanzania na kushindana katika masoko ya kikanda, kama inavyooneshwa katika vielelezo vifuatavyo.





Chanzo: Wizara ya Viwanda na Biashara na makadirio ya uzalishaji yaliyotolewa na makampuni

Maendeleo haya yanaonyesha kuwa uzalishaji wa ndani unakidhi mahitaji ya soko la ndani na viwanda hivi vina uwezo wa kuhudumia masoko ya kikanda. Hata hivyo, taarifa zinaonesha kuwa bidhaa za chuma na mabati bado zinaingizwa nchini, baadhi zikiwa na thamani ya chini isivyo kawaida. Hali hii inadhoofisha ushindani wa wazalishaji wa ndani, ukuaji wa viwanda, ajira, mapato na imani ya wawekezaji. Ili kuainisha maeneo ya kipaumbele kwa ajili ya kujadiliana na Serikali, Tarehe 10 Novemba 2026 Shirikisho la Sekta Binafsi (TPSF) lilifanya mjadala uliowakutanisha wazalishaji wa chuma na wadau wa sekta ya ujenzi, ambapo walikubaliana kuwa bidhaa za ndani zipewe kipaumbele kwa kuzingatia viwango vya ubora, huku bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ziendelee kuwekewa viwango vya kikodi vya juu ili kuweka uwiano wa ushindani kwenye soko.

2. Changamoto Kuu Zilizobainishwa

Uwiano wa Ushindani wa Bidhaa zinazoagizwa kutoka Nje ya Nchi nza zile zinazozalishwa ndani ya Nchi: Kuendelea kuingizwa nchini kwa bidhaa za chuma, ikiwemo kupitia ushushaji wa thamani (undervaluation), kunadhoofisha ushindani wa wazalishaji wa ndani licha ya kuwepo kwa uwezo wa kutosha wa uzalishaji nchini.

Upendeleo Usiotosheleza kwa Ununuzi wa Bidhaa za Ndani: Licha ya kuwepo kwa masharti ya ununuzi wa umma yanayotoa upendeleo wa asilimia 15 kwa bidhaa zinazozalishwa nchini, bidhaa za chuma za ndani hazipewi kipaumbele cha kutosha katika miradi ya ujenzi na miundombinu, hali inayopunguza fursa ya soko kwa wazalishaji wa ndani.

Mrundikano wa Tozo za Mamlaka za Udhibiti: Ada za ziada za mamlaka za udhibiti na mawakala, zikiwemo ada za TASAC (dry bulk cargo Minimum agency fees) na Ada zinazotozwa na Mamlaka ya Mapato (Customs Processing Fee), zinaongeza gharama za uendeshaji kwa wazalishaji na zinahitaji kufanyiwa mapitio

3. Mapendekezo ya Kisera

TPSF inapendekeza mapendekezo yafuatayo ya kisera ili kulinda sekta ndogo ya chuma nchini Tanzania:

Eneo la Sera	Pendekezo
Ushindani wa haki dhidi ya bidhaa za chuma zinazoingizwa kutoka nje ya nchi	Kuendeleza na mfumo wa sasa wa kodi kwa bidhaa za chuma zinapoingizwa kutoka nje ya nchi, kuanzisha bei ya chini ya Uingizaji bidhaa (Minimum Import Price) kwa bidhaa zote za chuma zinazoingizwa nchini ili kudhibiti ushushaji wa thamani, na kuongeza Ushuru wa Maendeleo ya Viwanda (IDL) kwenye mabati kutoka asilimia 5 hadi asilimia 10
Ununuzi wa Bidhaa Zinazozalishwa Nchini	Kusajili chuma kinachozalishwa nchini katika orodha ya bidhaa kwenye mfumo wa NeST ya PPRA, na PPRA inaombwa kufuatilia utekelezaji wa upendeleo huo katika mikataba ya kazi za ujenzi na kutoa mwongozo pale inapohitajika
Kupunguza gharama za uzalishaji zinazotokana na ada mbalimbali zinzotozwa na taasisi za udhibiti	Kupunguza gharama za kufanya biashara kwa Wazalishaji kwa kusamehe malighafi za wazalishaji kwenye tozo ya CPF inayotozwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania na kuangalia namna ya kufanya maboresho kwenye tozo za uwakala zinazotozwa kwa kupitia kanuni inayosimamiwa na Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC)

4. Hitimisho

Tanzania imepiga hatua kubwa katika kujenga tasnia yake ya ndani ya chuma. Kwa hiyo, TPSF inahimiza sera zitakazoimarisha mafanikio haya kwa kuhakikisha ushindani wa haki, uthamini sahihi na utozaji kodi stahiki kwa bidhaa zinazoingizwa nchini, pamoja na mifumo ya ununuzi inayotoa kipaumbele kwa bidhaa za chuma zilizozalishwa nchini.